katika agano jipya wapo watu wanne ambao wametajwa kwa jina la Yohana.. Wawili kati ya hao ndio hujulikana sana...ambao ni Yohana mbatizaji na Yohana mtume wa Yesu ..hawa wametajwa Sehemu nyingi katika agano jipya..

1) Yohana Mbatizaji

Mfano vifungu ambavyo utamsoma Yohana mbatizaji ni kama vifuatavyo:

- (Luka 1) – Kama mwana wa Zekaria na Elisabeti
- (Mathayo 3:13-17), Kama aliyembatiza Yesu
- (Marko 6; 14-29)- Kama aliyekatwa Kichwa na Herode.

2) Yohana mtume.

Hivi ni vifungu vinavyomtaja Yohana Mtume;

- (Mathayo 10:2) – Kama mmoja wa mitume 12 wa Yesu
- (Marko 1:19) Kama ndugu wa Yakobo, na mwana wa Zebedayo

Na ndiye mwandishi wa injili ya Yohana, pia na nyaraka zote tatu (1,2, 3 Yohana,) pamoja na kitabu cha Ufunuo.

3) Marko (Msaidizi wa huduma ya Paulo na Barnaba)

Yohana mwingine ni Marko, ndiye mwandishi wa kitabu cha Marko,..anatajwa katika kitabu cha Matendo 12:12, 13:5, Wakolosai 4:10

Na ndiye aliyekuwa Msaidizi wa Paulo na Barnaba katika ziara zao za kupeleka injili kwa mataifa.

4) Yohana babaye Petro

Yohana mwingine ni Baba wa Simoni Petro anatajwa katika;

Yohana 1:42

> *[42]Akampeleka kwa Yesu. Naye Yesu akamtazama, akasema, Wewe u Simoni, mwana wa Yohana; nawe utaitwa Kefa (tafsiri yake Petro, au Jiwe).*

Soma pia Yohana 21:15-27

Hivyo jumla Yao ni wanne...

Je ungependa kufahamu Zaidi watu wengine Katika biblia? Kama ni ndio basi jiunge tazama chini kwa makala nyingine..

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://chat.whatsapp.com/L3ysoFZcz058XCX9oLvKL1?s=cl&p=a&mlu=4&ilr=4

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

> *Filipo ni nani na je! Kuna Filipo wangapi katika biblia?*

> *Maherodi walikuwa ni akina nani, Na kazi yao ilikuwa ni ipi?*

> *Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.*

Share on:
WhatsApp